# DHANA ZA MSINGI NA MBINU ZA DORIA KWA VIJIJI VINAVYOTEKELEZA MKUHUMI (DRAFT)

Imeandaliwa na

VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED  P O BOX 349, LINDI

## DHANA MUHIMU KATIKA KANUNI ZA MKUHUMI

**Utangulizi**

MKUHUMI ni mfumo ulioanzishwa awali na Umoja wa Mataifa ambao una lengo la kuwapa motisha wamiliki wa misitu kulinda misitu yao. MKUHUMI ni kifupi cha "Kupunguza Uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na Ufyekaji na Uharibifu wa Misitu". MKUHUMI hupimwa kwa kutumia krediti za kaboni. Krediti 1 ni sawa na tani moja ya kabonidioxide. Kredit za kaboni hutolewa dhidi ya viwango vya kimataifa na kuuzwa katika sajili za kimataifa. Wanunuzi wengi ni makampuni ambayo hununua krediti za kaboni ili kufidia uzalishaji wa kabonidioxide kwenye shughuli zao.

### Dhana 10 za Msingi katika Miradi ya MKUHUMI

**Dhana ya 1: MKUHUMI inahusu kulinda misitu ya asili.**

Mpango wa MKUHUMI unahusu kulinda misitu, sio upandaji miti. MKUHUMI inatekelezwa kwenye Misitu ya Asili yanye umri wa miaka 10 au zaidi. Msitu in eneo la ardhi lenye ukubwa wa nusu hekta (ekari 1.2), na ambalo angalau 10% limefunikwa kivuli cha mitu, au miti iliyopo ina uwezekano wa kufunikwa na kivuli cha miti kwa zaidi ya 10% na kwamba miti iliyopo ina uwezekano au imefikia angalau urefu wa meta 3 inapoanza kukomaa.

**Dhana ya 2: MKHUMI inahusu kupambambana na matishiso ya ufyekaji na uharibifu wa misitiu**

MKUHUMI unatakelezwa kwenye misitu iliyo katika hatari ya kuharibiwa au kufyekwa. MKUHUMI unahusu kupunguza ukataji miti hovyo na/au uharibifu wa misitu. Hii ni kwa sababu motisha ya MKUHUMI inalipwa pale tu ambapo, msitu haukukatwa hovyo au kuharibiwa kutokana na uwepo wa motisha hiyo. Ni vigumu kuthibitisha kuwa Misitu ambayo haipo katika hatari ya kufyekwa au kuharibiwa, inaweza kukatwa endapo MKUHUMI haijatekelezwa kwenye eneo hilo.

| MKUHUMI | Miti ya kupanda |
|---|---|
| **Kredit za karbon hupatikana kupitia kupunguza ufyekaji wa misitu ya asili** | Kredit za karboni hupatikana kupitia miti ya kupanda |
| **Msitu wa asili unapaswa kuwa na umri wa miaka 10 au zaidi** | Eneo linalopandwa miti halipaswi kuwa na msitu kwa kipindi cha miaka 10 au zaidi iliyopita |
| **Mauzo ya Kredit za karbon yanapaswa kuwa sehemu ya motisha ya kuhifadhi** | Mauzo ya Kredit za karboni yanapaswa kuwa sehemu ya motisha ya kupanda miti |

**Dhana ya 3: Ridhaa huru:**

Dhana ya ridhaa huru katika mpango wa KUHUMI imejengwa katika misingi mitatu kama ifuatavyo

a) **Huru:** Kwamba hairuhusiwi kutumia nguvu, udanganyifu, unafiki, vitisho, lugha za kuudhi au aina yoyote ya kushurutisha katika kupata ridhaa ya watu kwa ajili ya tenga maeneo yao ya misitu na kuyahifadhi kwa ajili ya MKUHUMI. Endapo wakisema 'Hapana' haifai kuwashurutisha.

b) **'Ridhaa Kabla':** Dhana hii imejengwa katika misingi kuwa, shughuli zozote za MKUHUMI haziwezi kutekelezwa kabla ya kupata ridhaa ya watu wanahusika na msitu huo. Inahimizwa ridhaa hii iwe imetoka kwa makundi yote ya jamii, vijana, wazee wanawake, wanaume na watu wenye ulemavu.

c) **Elimu ya kutosha:** Kwamba elimu ya kutosha iwe imetolewa kwa makundi yote ya jamii, ikiwa ni pamoja na sera, sheria, kanununi na miongozo yote inayohusiana na MKUHUMI

d) **Maamuzi huru:** Kwamba wananchi kupitia vyombo vyao vya maamuzi yaani mkutano mkuu wa Kijiji wenye akidi sahihi watafanya maamuzi yoyote yanayohusiana na MKUHUMI kwenye maneo yao. Mchakato wa maamuzi unahimiza kuzingatia dhana ya kuwasikiliza kwa kina hata walio wachache na kuheshimu maamuzi ya wengi.

Dhana hizi zinapaswa kuzingatiwa katika michakato yote, tangu kufanya mpango wa matumizi ya ardhi ya Kijiji, kutenga maeneo ya hifadhi kwa ajili ya MKUHUMI, kufanya shughuli za ulinzi wa msitu, kufunga mikataba, kuandaa maandiko ya mradi, kufanya ufuatiliaji na tathmini, ukaguzi huru na kusajili kredit za kaboni, kufanya mauzo ya krediti za kaboni, na kugawana mapato au faida za MKUHUMI.

**Dhana ya 4: Ahadi wa Muda Mrefu:**

Ili MKUHUMI itekelezeke ni lazima wamiliki wa misitu waweke ahadi ya muda mrefu, kipindi kisichopungua miaka 30, kuthibitisha kuwa msitu utaendelea kuhifadhi. Ahadi hii lazima ithibitishwe katika mkataba na kuambatanishwa na vielelezo kamili. Endapo mmiliki wa msitu ataweza kuthibitisha kwamba msitu utahifadhiwa kwa muda mrefu zaidi inaweza kuongeza thamani ya kredit za kaboni zitakazopatikana.

**Dhana ya 5: Makadirio-msingi ya ufyekaji na uharibifu wa misitu**

Ili kupima kiwango cha kupungua kwa ukataji miti hovyo na uharibifu wa msitu, ni lazima kufanya uchambuzi wa kisayansi ili kukadiria ni hekta au ekari ngapi za msitu wa asili, wenye miaka 10 au zaidi zinaweza kupotea kwa mwaka endapo shughuli za uhifadhi hazitafanyika. Makadirio yanazingatia mambo makubwa mawili

a) Kiwango cha ukataji miti hovyo na uharibifu wa kihistoria katika msitu huo.


b) Ukaribu na matishio (visababishi) vya ukataji miti hovyo na uharibifu wa misitu

Misitu iliyokuwa na kiwango kikubwa cha ukataji miti hovyo na uharibifu wa msitu na ambayo imezungukwa na matishio au visababishi vingi inakuwa na makadirio-msingi makubwa.

Mfano huu unaonesha kuwa msitu uliokuwa na hekta 5712.9, umeonekana kuwa na makadirio msingi ya jumla ya hekta 634.5 kwa kipindi cha miaka mitano (2021– 2025)


| | Ekari | Uwiano | Makadirio |
|---|---|---|---|
| | 130.6 | 0.0006 | 0.1 |
| | 576.6 | 0.0131 | 7.6 |
| | 1279.1 | 0.0369 | 47.2 |
| | 1335.7 | 0.0779 | 104.1 |
| | 1448.1 | 0.135 | 195.5 |
| | 574.9 | 0.2178 | 125.2 |
| | 239.7 | 0.3402 | 81.5 |
| | 128.2 | 0.5714 | 73.3 |
| Total | 5712.9 | | 634.5 |

2021- 2025



**Dhana ya 6: Ufuatiliaji wa ukataji miti hovyo na uharibifu halisi wa misitu**

Hii ni upimaji wa matokeo halisi ya uhifadhi ambayo ni kupungua kwa kasi ya ukataji miti hovyo na uharibifu wa misitu. Dhana hii inasisitiza matumizi ya picha za angani (satelaiti), na ufuatiliaji halisi kwenye msitu ambapo kila eneo lililokuwa na msitu na au miti ya asili kwa kipindi cha tangu miaka 10 iliyopita ambalo litafyekwa au kuharibiwa litapimwa.



**Dhana ya 7: Kiasi cha kaboni kwenye msitu**

Katika eneo hili, kamati ya maliasili kwa kushirikiana na wataalamu wa misitu inapima miti katika vitalu kwenye

a) Eneo la Msistu wa Hifadhi wa Kijiji na

b) Kwenye maeneo ya mstitu wa hifadhi wa Kijiji yaliyofyekwa

Kisha wataalamu wa misitu na kredit za kabini hutumia milinganyo ya allometriki ili kubainisha uzitohai wa miti kwa kila ekari moja. Kisha wanakokotoa kiasi cha Uzalishaji wa Kabonidioxide kwa ekari moja iliyofyekwa ambayo inakuwa ni sawa na **(uzitohai wa miti kwa ekari moja ya msitu – uzitohai wa miti kwa ekari moja iliyofyekwa) * 0.5 * 44/12**;


ambapo 0.5 ni uwiano wa kaboni katika uzitohai wa mti na 44/12 ni uwiano wa uzito wa molekuli moja ya CO2 kwa molekuli moja ya C.

Tathmini ya mwaka 2015 ilionesha kuwa, Uzalishaji wa Kabonidioxide kwa ekari moja iliyofyekwa katika Mkoa wa Lindi ni tani 65.4 wa CO2 (tCO2e).

**Dhana ya 8: Krediti za bima au Akiba**

Ni lazima kuweka asilimia ya krediti za karboni za MKUHUMI kwenye akaunti ya akiba kwa ajili ya kama bima iwapo mradi utafeli. Miradi ya MKUHUMI hutumia kanuni ya kitaalaumu ijulikanayo kama "***AFOLU Non-Permance Risk Tool"*** kubainisha asilimia ya krediti za karboni ambazo huwekwa kwenye akaunti ya akiba. Kanuni hii kinaangalia matishio mbalimbali kama yanayohusiana na usimamizi, kifedha, kijamii, kisheria na kimazingira kwa mradi. Kiwango cha chini cha akiba ni 10%.

**Dhana ya 9: Uvujaji**

| | |
|---|---|
| Uvujaji hutokea wakati ufyekaji msitu ambao ungetokea katika eneo la mradi wa MKUHUMI unapohamia eneo lingine. Uvujaji hupimwa kwa kutumia misitu iliyo nje ya eneo la mradi, na hutokea endapo ufyekaji wa misitu iliyo nje ya eneo la mradi umevuka kiasi cha makadirio-msingi. Uvujaji = idadi ya ekari zizokadiriwa kufyekwa nje ya eneo la mradi – idadi halisi ya ekari zilizofyekwa nje ya eneo la mradi. |   |

**Dhana ya 10: Soko huru**

Soko la hiari la krediti za karboni ambazo huzalishwa na kuuzwa kwa hiari. Wanunuzi wakubwa ni kampuni zinazotafuta kufikia malengo yao ya hiari kama sehemu ya majukumu ya kampuni. Hatua hizi ni pamoja na kanuni za utoaji wa hewa chafu katika nchi yao. Krediti za karboni mara nyingi ni moja tu ya shughuli kadhaa wanazofanya ili kupunguza uzalishaji. Wananunua krediti kwa sababu inaongeza thamani kwa biashara yao

## MBINU ZA MSINGI KATIKA DORIA YA MSITU UNAOTEKELEZA MKUHUMI

### Utangulizi

MKUHUMI ni kifupi cha **"Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na ukataji miti hovyo (ufyekaji) na Uharibifu wa Misitu".** MKUHUMI ni mfumo ulioanzishwa awali na Umoja wa Mataifa ambao una lengo la kuwapa motisha wamiliki wa misitu kulinda misitu yao. MKUHUMI unatekelezeka kwenye misitu ya asili yenye umri zaidi ya miaka 10 na ambayo ipo katika hatari ya kufyekwa/kukatwa hovyo. Motisha ya MKUHUMI inaweza kulipwa kutokana na kutimiza malengo ya uhifadhi kwa i) Kupunguza ufyekaji ya misitu, yaani kupunguza kasi ya kubadilisha sehemu au eneo la msitu wa hifadhi wa Kijiji kuwa matumizi mengine ya ardhi kama vile mashamba na makazi na ii) Kupunguza uharibifu, yaani kupunguza shughuli ambazo zinapunguza ubora wa msitu wa hifadhi kama vile uvunaji haram una usio endelevu, na uchomaji moto hovyo. Maswala yote yanayohusiana na maamuzi juu ya MKUHUMI yenajengwa katika dhana ya **Ridhaa Huru**, hivyo malengo makuu ya doria ya msitu unaotekeleza mpango wa MKUHUMI yanapaswa kuzingatia

i) Kutoa elimu ya uhifadhi na MKUHUMI kwa watu anaotuhumiwa muharibu msitu wa hifadhi wa Kijiji
ii) Kulinda msitu na au/ miti ya asili yenye umri wa miaka 10 au zaidi ndani ya Msitu wa Hifadhi wa Kijiji

### Mbinu za udhibiti wa msitu wa hifadhi wa Kijiji kwa ajili ya kunufaika na MKUHUMI


**Mbinu Kwanza: Kubainisha mipaka na kuweka alama za kudumu na zinazoonekana**.

Katika hatua hii Kijiji kinaweza kuhakiki mipaka ya msitu wa hifadhi wa Kijiji ili kuhakikisha kuwa alama za mipaka zilizopo kwenye ramani, zinawiana na alama halisi. Aidha ni muhimu kuhakikisha kuwa eneo lote la msitu lililohifadhiwa kwa ajili ya biashara ya kaboni halina mgogoro wowote. Vile vile ni muhimu kuhakikisha kuwa maeneo yote yam situ yaliyo nje ya msitu wa hifadhi wa Kijiji na ambayo hayo katika hatari ya kufyekwa kwa ajili ya kilimo na makazi au matumizi mengine yanahifadhiwa. Baada ya kuhakiki mipaka Kijiji kinapaswa kuweka lama za kudumu na zinazoonekana, yaani

a) Kusafisha mipaka kwa kufyeka barabara inyozunguka msitu wa hifadhi wa Kijiji
b) Kuweka alama za kudumu kama vile mabango na bikoni

**Mbinu ya pili: Uchambuzi wa picha za angani/satelaiti**

Katika hatia hii *Village Climate Solutions Limited (VCSL)* itakuwa na wataalamu wa miumo ya kidunia ya picha za angani (GIS) ambao watasaidia kukusanya na kuchambua picha za angani za msitu wa hifadhi wa kijiji na kutoa taarifa kwa Kikosi cha Doria kwa njia ya simu maalum kila mwezi. Kwa kutumia teknolojia hii eneo lolote la msitu wa hifadhi wa kijiji litakalofyekwa litaweza kubainika na kuwekwa bayana mara moja. VCSL itakuwa inatoa taarifa hizi kwa kikosi cha doria cha Kijiji ambacho kitatumia technolojia ya ramani za kwenye simu kufuatilia sehemu ambayo picha za satelaiti zimeonesha kuwa ina uharibifu ili waweze kuchukua hatua mapema. Na wazi kuwa kwa kutumia mfumo huu,  sehemu yoyote ya msitu wa hifadhi itakayofyekwa lazima itabainika.







**Mbinu ya tatu: Kuunda Timu Doria ya Kijiji**

Kila Kijiji kinachotaka kunufaika na biashara ya kaboni kupitai mfumo wa MKUHUMI, lazima kihakikishe kinakuwa na timu nzuri ya doria, ambayo inatekeleza wajibu wake ipasavyo. Timu doria lazima iundwe kupitia mkutano mkuu wa Kijiji na kuwa na uwakilishi kutoka kwenye vitongoji, hususani vile ambavyo vipo karibu zaidi na msitu wa hifadhi wa Kijiji. Timu doria itawajibika kwenye kamati ya maliasili, ambayo itakuwa inawajibika kwenye halmashauri ya Kijiji na mkutano mkuu wa Kijiji ndiyo utakaokuwa na maamuzi ya mwisho kuhusu shughuli zinazofanywa na timu doria.

**Mbinu ya nne: Kufanya doria na kuweka kumbukumbu kwa kutumia technolojia ya simu na picha za angani**

Kazi kubwa ya timu doria itakuwa ni kuhakikisha kuwa msitu wa hifadhi wa Kijiji unalindwa ili kuepusha ufyekaji au ukataji miti hovyo na uharibifu mpya hautokei. Timu doria itakuwa

inatumia technilojia ya simu zenye mfumo wa picha za angani kufanya doria kwenye maeneo yaliyobainika kuwa katika hatari ya kufyekwa au yeliyoonekana kufyekwa baada ya kuanza kwa mradi. Vile vile timu doria itakuwa inatumia tchnolojia ya simu kukusanya, kuhifadhi, na kuchakata taarifa za doria

**Utaratibu wa kuweka kumbukumbu za doria kwa kutumia simu**

Timu ya doria itakuwa inatumia app ya ***Mergin Maps*** kukusanya, kuhifadhi na kuchakata taarifa za doria kila mwezi. Mergin Map itasaidia timu ya doria kupokea taarifa za hivi karibuni kuhusu msitu na GPS ya kwenye simu itawasaidia kutembelea maeneo yenye uharibifu kwa ajili ya uhakik, kukusanya taarifa muhimu na kuchukua hatua za kuzuia uharibifu huo usiendelee. App ya ***Mergin map***s imekwishahifadhiwa kwenye simu za timu ya doria na kusajiliwa kwa ajili ya matumizi.

**Hatua ya kwanza:** Fungua app ya ***Mergin maps*** kwenye simu yako, kisha nenda kwenye sehemu ya miradi iliyoshirikishwa (*shared projects*), kufungua mradi unaohusika na Kijiji chako. GPS ya kwenye simu itakuelekeza kwenda kwenye eneo la mradi ambalo uharibifu unaonekana.

**Hatua ya pili:** Jaza taarifa za msingi zinazohusiana na uharibifu kama inavyoonekana kwenye dodoso. Kumbuka baada ya kujaza takwimu zote zinazohitajika utathibitisha kuwa umekamilisha kwa kujaza ***(ndiyo)*** sehemu ya “Rekodi imekamilika”? Kisha fanya yafuatayo

***a)*** Hakikisha ramani imekuonesha kuwa upo ndani kabisa ya eneo lenye uharibifu

***b)*** Hakikisha umechagua GPS ili kumbukumbu za jira ya eneo husika kutoka kwenye GPS

***c)*** Usahihi wa GPS uwe chini ya mita 5

***d)*** Ekari zilizofyekwa zitaonekana moja kwa moja kwenye fomu

***e)*** Hakiki tarehe na muda wa doria

***f)*** Weka maelezo ya ziada kuhusu uharibifu huo kama yapo

**Hatua ya tatu: Kukusanya na kuhifadhi taarifa za kina kuhusu Makosa:**

a) Weka kumbukumbu za makosa yaliyofanyika kwa kuchagua kwenye orodha. Unaweza kuchagua kosa zaidi ya moja, kisha chagua sababu kuu ya makosa hayo kama inavyoonekana kwenye orodha, kisha fuata maelekezo ya maswali mengine kama inavyoonekana.

**Hatua ya nne: Uchambuzi wa kina kuhusu Mkosaji ikijumuisha,**

a) Majina yake kamili, namba yake ya simu, umri wake, kiwango chake cha juu cha elimu na jinsi yake
b) Makazi yake, ili kujua kama anatoka Kijiji cha mradi, Kijiji Jirani, sehemu nyingine ndani ya wilaya, nje ya wilaya au mkoa tofauti.
c) Umiliki wa ardhi, yaani kama alijua yuko ndani ya mipaka ya msitu wa hifadhi wa Kijiji au la, na kwamba kama anamiliki ardhi nyingine nje ya msitu wa hifadhi wa Kijiji
d) Hatua zilizochukuliwa ikiwa ni pamoja na kujua kama ni kosa lake la kwanza au la, na serikali ya Kijiji ilichukua hatua gani dhidi ya uhalifu huu.

Takwimu zitakazoklusanywa zitasaidia kuandaa andiko la mradi, kuandaa taarifa msingi za mradi, na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya kuthiobitisha kredit za kaboni zitakzaozalishwa.

**Mbinu ya tano: Elimu kwa jamii**

Mamuzi yote yanayohusiana na MKUHUMI yanatawaliwa na dhana ya ridhaa huru (FPIC). Ili kutekeleza dhana hii, swala la elimu kwa jamii hasa ambayo inafanya shughuli zake kando kando ya Msitu wa Hifadhi wa Kijiji linapewa kipaombele. Hivyo moja ya kazi kubwa ya Timu doria ni kutoa elimu hii kupitia mikutano ya jamii. Jambo la msingi la kuelewa ni kwamba, si lengo la MKUHUMI kuhamisha watu kwenye maeneo ambayo tayari yamekwishavamiwa, kwani mpango huu unatekelezeka kwenye misitu ya asili, yenye umri wa miaka 10 au zaidi. Hii ina maana kwamba, maeneo yote ambayo tayari yalikwishafyekwa ndani ya miaka 10 iliyopita sio kipaombele kwa ajili ya MKUHUMI. Lengo la MKUHUMI ni kuzuia ufyekaji na uharibifu mpya usitokee kwenye maeneo ambayo yalikuwa msitu kwa kipindi cha mika 10 iliyoyopita au zaidi. Kwa kutumia teknolojia ya picha za satelaiti, ni wazi kwamba ufyekaji au uharibifu mpya utagunduliwa popote pale utakapofanyika. Aidha Timu doria itawaelimisha wanajamii kuwa, endapo ufyekaji au uharibifu mpya utatokea kwenye msitu wa hifadhi ni hasara kubwa, kwani watakuwa wanapoteza mapato ya MKUHUMI kwa kila eneo jipya litakalokuwa linafyekwa. Vile vile ni muhimu kusisitiza kuwa mbali na mapato ya MKUHUMI, kufyeka msitu kuna hasara nyingine kwani misitu ina faida nyingine kama  mbao, nguzo/fito/majengo, kuni, chakula, asali, kuhifadhi vyanzo vya maji na kuboresha hali ya hewa kwenye maeneo yao.

**Mbinu ya sita: Matumizi ya Kibali**

Utaratibu uliozoeleka wa vibali unaweza kuendelea kutumika endapo kuna shughuli nyingine zitakuwa zinafanyika kwenye msitu wa Hifadhi wa Kijiji. Kibali ni mbinu ya kuhakikisha kuwa, yeyote aliyeruhusiwa kufanya jambo ambalo limekatazwa kufanyika kwa mujibu wa sheria anakuwa na vielelezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria, kuthibitisha kuwa yeye ameruhusiwa. Kibali huweka masharti ya mipaka ya kufanya jambo lililoruhusiwa kwa mujibu wa kibali hicho. Kibali husaidia kutofautisha kati ya walioruhusiwa kwa mujibu wa sheria, na wale wanaotaka kufanya jambo lililokatazwa bila kuzingatia utaratibu uliowekwa. Kibali huisaidia serikali ya kijiji kudhibiti matumizi ya rasilimali kwa mujibu wa sheria. Kibali kinapaswa kuwa na sehemu zifuatazo;

| **Sehemu ya Kibali** | **Ufafanuzi** |
|---|---|
| Utambulisho | Jina, Nembo na anuani ya mamlaka unayotoa kibali hicho |
| Kichwa cha Habari | Inaeleza kibali hicho kinatolewa kwa ajili ya nini? Mfano; KIBALI CHA KURINA ASALI KWENYE ENEO LA CHANZO CHA MAJI |
| Namba ya Kibali | Onesha Kibali hicho ni namba ngapi na kimetolewa mwaka gani |
| Tarehe | Andika Tarehe ya kutolewa Kibali |
| Aliyepewa Kibali | Huonesha jina, anunani, namba ya simu na namba nyingine za kumtambulisha aliyepewa kibali. Huonesha kama kibali kimetolewa kwa mtu, kikundi cha watu, au taasisi. |
| Nukuu ya Sheria | Huonesha kifungu cha Sheria au Kanuni zilizoweka utaratibu wa kutoa kibali hicho |
| Muda wa kibali | Huonesha tarehe ya kuanza kutumika kwa kibali hadi tarehe ya mwisho au ukomo wa kibali hicho |
| Masharti ya kibali | Huonesha kwa kifupi mambo ambayo yakikiukwa hupelekea ukomo wa kibali hicho au adhabu mbalimbali zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za serikali ya kijiji au sheria za nchi |
| Mtoaji wa kibali | Huonesha jina, cheo na saini ya aliyotoa kibali hicho, na tarehe alipokikabidhi kwa mhusika |
| Mhuri | Kibali lazima kipigwe mhuri wa taasisi inayohusika na kibali hicho |

Nakala zisizopungua mbili za kibali kinachotolewa zinapaswa kuandaliwa; ambapo nakala halisi (original) atapewa aliyeandikiwa kibali hicho, na nakala moja itabaki katika ofisi ya kamati inayohusika na kibali au halmashauri ya kijiji kwa ajili ya uhakiki, ukaguzi na rejea.

Katika kamati ya maliasili, wizara ya maliasili na utalii iliandaa vitabu maalumu vya vibali vya kuingia msituni. Ufutao ni mfano wa kibali cha kuingia msituni

**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA ________________________________**
**KAMATI YA MALIASILI YA KIJIJI**

**KIBALI CHA KUINGIA KATIKA MSITU WA HIFADHI WA KIJIJI CHA_____________________**
**KIBALI NAMBA__________ CHA MWAKA_______________________**
Tarehe_______________________
Kibali kimetolewa kwa _________________________________ wa ___________________

Kwa Masharti yaliyo katika Sheria Ndogo za kutunza, kusimamia Msitu wa Hifadhi wa Kijiji cha __________________________ya mwaka ______, na kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za kuhifadhi maliasili Tanzania,;
(Jina) _______________________________ameruhusiwa/wameruhusiwa kuingia katika Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kwa ajili ya ___________________________________________________________ ____________________________________________________________________________________
Kibali hiki kitaanza kutumia tarehe _________________mwezi _____________ mwaka _________
Kibali hiki kitakoma kutumika tarehe _________________ mwezi ___________ mwaka _________

**MASHARTI YA KIBALI HIKI**

- ❖ Mwenye kibali haruhusiwi kufanya shughuli nyingine tofauti na zilizoainishwa kwenye kibali
- ❖ Mwenye Kibali ataongozana na mjumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji au mwenyeji mwingine aliyeruhusiwa na kamati ya maliasili ya kijiji wakati atakapoingia kufanya shughuli zake kwenye msitu wa hifadhi wa kijiji
- ❖ Mwenye kibali endapo si raia wa Tanzania, atatakiwa kuonesha vielelezo vyote vya kuingia nchini, ikiwa ni pamoja na shughuli aliyokuja kufanya
- ❖ Mwenye kibali haruhusiwi kuzidisha muda zaidi ya uliooneshwa kwenye kibali, na kama atafanya hivyo ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za kutunza, kusimamia Msitu wa Kijiji za mwaka __________.

Jina la Mtoa Kibali _____________________Cheo________sahihi _________Tarehe ___________
**MHURI**

**Mbinu ya saba: Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Mkosaji**

Kama ilivyokuwishaelezwa awali, kanuni za viwango vya MKUHUMI zinasisitiza ridhaa huru, katika kila hatua ya maamuzi. Hivyo, katika kuchukua hatua dhidi ya mkosaji, ni vema kuzingatia mbinu zifuatazo

***a)*** **Elimu kwa Mtuhumiwa**: Timu doria itapaswa kuhakikisha kuwa, hatua ya kwanza kabisa ya kushughulika na mtuhumiwa ni kumpa elimu, kwamba

- **i)** Aelezwe shughuli anazofanya ni kinyume na Sheria Ndogo za kuhifadhi msitu wa Kijiji na asomewe vifungu vya Sheria alivyokiuka,
- **ii)** Ahimizwe kwamba shughuli anazofanya zinasababisha uharibifu na upotevu wa rasilimali za Kijiji kama mbao, nguzo/fito/majengo, kuni, chakula, asali, kuhifadhi vyanzo vya maji na kuboresha hali ya hewa kwenye maeneo yao,
- **iii)** Ahimizwe kuwa shughuli anazofanya zinasababisha Kijiji kukosa mapato ya MKUHUMI, ambayo ni mfumo wa motisha ya kibishara, kwa Kijiji kinachopunguza ukataji miti hovyo na uharibifu wa misitu,
- **iv)** Aelezwe kwamba lengo la MKUHUMI ni kuhakikisha kuwa hakuna ukataji miti hovyo na uharibifu mpya wa misitu yote yenye umri wa miaka 10 au zaidi, ndani ya mipaka ya Msitu wa Hifadhi wa Kijiji,
- **v)** Ashauriwe kuwasiliana na uongozi wa serikali ya Kijiji anapotaka kufungua shamba jipya, ili aoneshwe maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kilimo, kupitia mpango wa matumizi ya ardhi wa Kijiji,
- **vi)** Ahamasishwe kwamba MKUHUMI ina lengo la kuhimiza mbinu bora za kilimo, kama matumizi ya pembejeo bora, ili kuongeza uzalishaji kwenye eneo dogo, hivyo kuna wataalamu wa kilimo wanaweza kumsaidia.
- **vii)** Aahidi kwamba atasitisha shughuli zozote zile zinazohusiana na ukataji miti hovyo na uharibifu wa misitu kwani ni hasara kwake na kwa jamii nzima.

***b)*** ***Onyo na karipio kwa mkosaji:*** Onyo linaweza kutolewa kama hatua ya pili ya kushughulika na mkosaji katika msitu wa hifadhi wa Kijiji. Onyo au Karipio linaweza kufananishwa na kadi ya njano kwenye mpira wa miguu, ambayo humtahadharisha mhusika kuwa akirudia tena kosa kama hilo anaweza kufukuzwa uwanjani kwa kupewa kadi nyekundu. Ni tamko au kauli ya kuonesha masikitiko na hasira dhidi ya makosa yaliyofanyika. Katika hatua hii, mkosaji au mtuhumiwa anapewa  tahadhari dhidi ya mwenendo usiofaa au unoaelekea kuvunja

sheria na kuharibu mafanikio yanayotarajiwa katika usimamizi wa rasilimali za kijiji. Onyo ni ushauri wa tahadhari kwamba tabia fulani ikiendelea, inaweza kusababisha hasara kwani itapelekea upotevu wa msitu wa hifadhi wa kijiji. Tamko la onyo litaonesha maelezo ya hali halisi, makosa yanayofanyika, madhara yake na mapendekezo ya nini kifanyike ili hasara inayotarajiwa iepukike. Kwa mfano, onyo linaweza kutolewa kwa kiongozi ambaye anaidhinisha wakulima wapya wafungue mashamba Ndani ya Msitu wa Hifadhi au kwenye eneo lililo karibu sana na Msitu wa Hifadhi wa Kijiji. Vile vile onyo linaweza kutolewa kwa mtu ambaye amekwishapatiwa elimu laikini shughuli zake zina mwelekeo ya kushababisha ukataji miti hovyo au uharibifu wa msitu wa Kijiji. Onyo linaweza kutolewa kwa mdomo, mfano kupitia vikao na kukumbukumbu zake kuandikwa kwenye muhtasari au kwa kuandikiwa barua.

***c) Kutakiwa kujieleza au kuomba radhi:*** Ni mbinu ya usimamizi wa sheria ambapo mkosaji hutakiwa kujieleza mbele ya mamlaka ya kinidhamu katika kamati au halmashauri ya kijiji. Mkosaji hutakiwa kutoa ufafanuzi wa makosa aliyoyafanya kwa maandishi mbele ya kikao chenye maamuzi dhidi yake, au mbele ya kamati maalum iliyoundwa. Kadhalika, mkosaji anaweza akatakiwa kuomba radhi kwa kuandika barua au kutoa kauli ya kuomba radhi mbele ya kikao cha kamati husika, cha halmashauri au hata mkutano mkuu wa Kijiji, na kumbukumbu zake zikawekwa kimaandishi. Katika kuomba radhi, mkosaji ataeleza masikitiko yake dhidi ya makosa aliyoyafanya na jinsi anavyojutia hasara aliyosababisha na kuahidi kwa dhati kwamba hatarudia tena.

***d)* Hati ya Kukiri kosa na kukubali adhabu**

Utoaji wa adhabu kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na serikali ya kijiji ni moja ya mbinu muhimu katika kulindi msitu wa hifadhi wa kijiji katika kusimamia utawala wa sheria. Adhabu zinazopaswa kutolewa ni zile zilizoainishwa kwenye sheria ndogo au maazimio halali ya serikali ya kijiji.

Hati ya kukiri kosa na kukubali adhabu ni mbinu ya menejimenti katika usimamizi wa sheria kwani huisaidia serikali ya kujiji kutunza kumbukumbu za ushahidi kwa wahalifu walioadhibiwa kwa mujibu wa sheria ndogo za kijiji. Hati ya kukiri kosa na kukubali adhabu, husaidia kuepuka mhalifu kukana makosa aliyokiri kuyafanya na kusingizia kuwa alionewa. Katika usimamizi wa sheria, wajumbe wote wanaofanya makosa katika serikali ya kijiji na kukubali adhabu, wanapaswa kusaini hati ya kukiri kosa na kukubali adhabu. Aidha ni muhimu kusisitiza hapa kuwa, tendo la kusaini hati ya kukiri kosa na kukubali adhabu haimaanishi adhabu imetekelezwa,

bali mhalifu amekubali kutekeleza adhabu hiyo, na kwamba ataitekeleza kwa kuzingatia masharti yaliyotolewa na kamati au halmashauri ya kijiji.  Hati ya kukiri kosa na kukubali adhabu inakuwa na sehemu zifuatazo.

| **Sehemu** | **Ufafanuzi** |
|---|---|
| Utambulisho | Jina, Nembo na anuani ya mamlaka unayotoa kibali hicho |
| Kichwa cha Habari | Mfano; HATI YA KUKIRI KOSA NA KUKUBALI ADHABU |
| Tarehe | Tarehe ambayo hati imeandaliwa |
| Namba ya hati | Namba ya hati kwa mtiririko kama zilivyopangwa kwenye kitabu |
| Utambulisho wa Mkosaji | Majina kamili, umri, jinsia, dini, kabila, anunani ya mkosaji |
| Tamko la kukiri kosa | Maelezo ya mhalifu akitamka makosa aliyoayafanya, kifungu cha sheria alichokiuka, akitamka wazi kukiri kutenda makosa hayo |
| Tamko la kukiri na adhabu | Maelezo ya mhalifu akieleza adhabu zinazomkabili, kifungu cha sheria kilichoweka adhabu hizo, akitamka wazi kuwa tayari kutekeleza adhabu zilizowekwa |
| Mkakati wa kutekeleza adhabu | Maelezo ya mhalifu akieleza jinsi atakavyotekeleza adhabu hiyo na tarehe ya mwisho kukamilisha adhabu aliyopewa |
| Saini ya Mkosaji | Jina na saini ya mkosaji, na tarehe aliyotia saini hati ya kukiri kosa na kukubali adhabu |
| Saini ya aliyetoa adhabu | Tarehe, Jina, cheo na saini ya aliyetoa adhabu |
| Mhuri | Mhuri wa kamati au halmashauri au kiongozi aliyetoa adhabu |

Aidha, kwa upande wa kamati ya maliasili, kuna vitabu maalumu vilivyoandaliwa na wizara ya Maliasili na utalii kwa ajili ya wahalifu wanaokiri makosa na kukubali adhabu kwa mujibu wa sheria ndogo za usimamizi wa msitu wa kijiji. Muundo wa hati ya kukiri kosa na adhabu ni kama ifuatavyo

**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA ______________________________**
**KAMATI YA MALIASILI YA KIJIJI**

**HATI YA KUKIRI KOSA NA ADHABU YA FAINI NA FIDIA**
Tarehe _______________
**Hati namba ___________________ ya mwaka _____________________**
Mimi ____________________________________________________________ Mkazi wa __________ nikiwa na akili timamu, nakiri chini ya Sheria Ndogo za kutunza, kusimamia Msitu wa Kijiji cha ______________ kutenda makosa yafuatayo tarehe ______________________ katika eneo ________________________;
1. _____________________________________________________________________
2. _____________________________________________________________________
3. _____________________________________________________________________
Kwa hiari yangu nakubali kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria ndogo za hifadhi ya msitu wa kijiji cha _____________________________
**Adhabu zilizotolewa**
1. _____________________________________________________________________
2. ______________________________________________________________________
Jina na Sahihi ya Mkosaji
Jina ________________________________ Sahihi _______________ tarehe __________
**ADHABU HII IMETOLEWA NA**
Jina ______________________________________ Cheo ________________________________
Sahihi ______________________________________ tarehe _______________________________
**MHURI**

e) ***Faini na fidia:*** Ni kiasi cha malipo ambacho mkosaji atatakiwa kulipa kwa mujibu ya sheria aliyovunja kwa kosa alilofanya. Kuendana na kosa lililofanyika na hali halisi ya mazingira ya kosa, na kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa na serikali ya kijiji, zaidi ya adhabu moja inaweza kutolewa kwa wakati mmoja. Tathmini ya uharibifu inaweza kufanyika na mkosaji anaweza kutakiwa kulipa hasara yote aliyosababisha.

f) ***Kufungua jalada la Kesi Polisi na Mahakamani***

Hii ni mbinu mojawapo ya menejimenti katika kusimamia sheria ndogo za kijiji, ambapo wahalifu wanaweza kufunguliwa majalada ya uchunguzi polisi na kufikishwa mahakamani kwa sababu mbali mbali kama vile;-

a) Endapo wamegoma kukubali adhabu walizopewa kwa mujibu wa sheria ndogo za kijiji

b) Endapo wamegoma au kushindwa kutekeleza adhabu walizokubali kwa mujibu wa sheria ndogo za kijiji

c) Endapo wamefanya makosa ambayo adhabu zake zipo nje ya mamlaka ya serikali ya Kijiji

d) Endapo imeonekana wazi kwamba wamekaidi kuzingatia elimu, fursa mbadala walizopewa na kwamba matendo yao yanaathiri maslali ya wengi bila sababu

### *g) Kitabu cha Orodha ya Makosa*

Kitabu cha orodha ya makosa ni mbinu nyingine ya menejimenti katika usimamizi wa sheria ndogo za usimamizi wa rasilimali za kijiji, ambayo inaweza kutumika kuweka kumbukumbu za uhalifu. Kitabu hiki kinatumika kwa ajili ya wahalifu wa ndani ya kijiji tu, yaani wakazi wa kijiji husika. Serikali ya kijiji inaandaa kitabu maalumu ambacho kila mkosaji atatakiwa kusaini katika kitabu hicho. Katika kitabu hicho mkosaji atatakiwa kuingiza taarifa zifuatazo

| **Taarifa atakazoingiza** | **Ufafanuzi** |
|---|---|
| Utambulisho | Mkosaji ataandika majina yake kamili, cheo chake na kitongoji anachotoka |
| Kosa alilofanya | Mkosaji atataja makosa aliyofanya akionesha vifungu vya sheria ndogo alizokiuka |
| Adhabu alizopewa | Mkosaji atataja adhabu zilizomkabili kutokana na kosa alilofanya, |
| Saini | Mkosaji ataweka saini yake na tarehe |

### *h) Kuweka Wazi Taarifa za Uhalifu na Adhabu*

Taarifa za uhalifu na adhabu zilizotolewa zinapaswa kuwekwa wazi kwa wananchi. Hii ni mbinu muhimu katika usimamizi wa rasilimali za kijiji, kwani husaidia kupunguza uhalifu/makosa. Wakosaji hasa wanapokuwa ni viongozi watafanya jitihada za kuepuka makosa wanapotambua kuwa makosa watayowanya yatajulikana kwa wananchi na kwamba wataonekana ndio waliosababisha hasara fulani kwa kijiji. Hali kadhalika wananchi watajitahidi kuepuka makosa mbalimbali kwa kutambua kuwa makosa yao yatajulikana wazi kwa jamii na kuwaletea aibu. Watendaji wa kijiji wanapaswa kuandaa taarifa za uhalifu uliofanyika kila mwezi na kila robo mwaka kwa ajili ya kuziwasilisha kwenye vikao na baadae kwenye mkutano mkuu wa kijiji. Taarifa za uhalifu itajumuisha

| **Kipengele cha Taarifa** | **Ufafanuzi** |
|---|---|
| Jina la Mkosaji | Eleza majina kamili ya mkosaji, cheo chake, na sehemu anayoyotoka |
| Makosa aliyofanya | Taja makosa aliyofanya ukionesha vipengele vya sheria aliyovunja |
| Adhabu alizopewa | Taja adhabu zote alizopewa ukionesha misingi ya sheria ndogo katika kutoa adhabu hizo, na jinsi alivyozitekeleza |

Taarifa inaweza kuandaliwa kwa mtiririko ufuatao

| No. | Jina la Mkosaji | Makosa aliyofanya | Adhabu alizopewa |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| | | | |

**Kufanya ufuatiliaji na tathmini**

Kama ilivyokwishaelezwa awali, Mradi wa MKUHUMI utafanya Ufuatiliaji na tathmini ya hali ya ukataji miti na uharibifu wa msitu wa Kijiji kila mwezi kwa kutumia picha za angani. Taarifa ya tathmini ndiyo itakayokuwa kipimo cha malipo ya MKUHUMI kwa Kijiji. Vile vile serikali ya Kijiji inaweza kutumia taarifa hizi kama kigezo cha kutathmini mwenendo mzima wa kazi zinazofanyika, na baadae kufanya tathmini ili kupima kiwango cha mafanikio katika usimamizi wa msitu wa hifadhi wa Kijiji.

a) Kupima kiwango cha uzingatiaji wa sheria zilizowekwa

b) Kutambua sheria zenye makosa na kuzirekebisha

Hii itasaidia kuhimiza uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria kwani watendaji na wanajamii watatambua kuwa, kuna watu au taasisi nyingine zenye mamlaka kubwa ambazo zinafuatilia na kuhakiki kazi zinazofanyika, na kutathmini kiwango cha uzingatiaji wa sheria zilizowekwa.

**Kuitisha Uchunguzi Maalum au Ukaguzi wa Nje**

Katika kutekeleza shughuli za MKUHUMI, serikali ya Kijiji inashauriwa kuepuka kuchukua hataua zozote dhidi ya jambo ambalo halina Ushahidi wenye vithibiotisho halali 9vilivyo kwa maandishi na kamili. Uchunguzi na ukaguzi katika utawala wa sheria ni mbinu ya menejimenti katika serikali ya kijiji yenye lengo la kutumia vyombo vyenye weledi na vinavyoaminika kubaini kiwango cha uhalifu au ukiukwaji wa sheria; kuonesha kasoro zilizopo kwenye sheria zinazotumiwa na serikali ya kijiji. Ukaguzi utasaidia kuthibitisha taratibu za uzingatiaji sheria na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala ya usimamizi wa sheria za kijiji. Watendaji wa kamati na halmashauri ya kijiji huongeza umakini katika utekelezaji wa kazi zao wanapotambua kuwa kazi wanazofanya zitakaguliwa.